**BARAZA LA WAWAKILISHI ZANZIBAR**

Simu Nam. + 255 24 2230602/1
Fax Nam. + 255 24 2230215
Tovuti: www.zanzibarassembly.go.tz

SANDUKU LA BARUA 902,
ZANZIBAR
Barua Pepe: zahore@zanlink.com

# HOTUBA YA MAONI YA KAMATI YA KUSIMAMIA OFISI ZA VIONGOZI WAKUU WA KITAIFA KUHUSU MSWADA WA SHERIA YA MAREKEBISHO YA SHERIA MBALI MBALI NA KUWEKA MASHARTI BORA NDANI YAKE

---

**Mheshimiwa Spika;** awali ya yote napenda kutumia nafasi hii kumshukuru Mwenyezi Mungu (S.W) kwa kutujaalia afya njema iliyotuwezesha kukutana tena leo hii kwa nia ya kuendeleza majukumu yetu ya msingi kwa nchi yetu kwa ujumla katika mkutano huu wa tisa. Ninamuomba Mwenyezi Mungu Mtukufu azidi kutukirimu neema zake ambazo kwa hakika sote ni wahitaji kwake.

**Mheshimiwa Spika;** aidha, naomba pia nikushkuru wewe binafsi Mheshimiwa Spika kwa kunipa nafasi hii ya kusimama mbele ya Baraza hili Tukufu kusoma machache juu ya maoni na mapendekezo kwa niaba ya Kamati yangu ya Kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa ya Baraza hili kuhusu Mswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria MbaliMbali na Kuweka Masharti Bora ndani yake.

**Mheshimiwa Spika;** shukurani za kipekee ziende kwa Mwanasheria Mkuu na watendaji wake wote wakiwemo wale ambao wameguswa ndani ya Mswada huu moja kwa moja, kusema kweli kamati yangu inakubaliana na madhumuni ya kuwasilishwa Mswada huu, mbele ya Baraza lako Tukufu kwa ajili ya kufanya Marekebisho ya Sheria hizo ili kwenda sambamba na malengo ya kuwepo kwa Sheria husika katika utekelezaji wake.

**Mheshimiwa Spika;** napenda pia, nitumie fursa hii kuwashukuru Wadau mbali mbali ambao Kamati yetu iliweza kuwashirikisha na kutoa maoni yao mbalimbali ili kupata michango bora katika utekelezaji, hiyo ikiwa ni hatua ya kuuboresha Mswada huu. Hata hivyo, Kamati inaishauri Ofisi ya Baraza kuweka kuratibu mapema namna ya kuwapata wadau ambao kwa kiasi kikubwa wanatusaidia kupata michango iliyo bora.

**Mheshimiwa Spika,** aidha, pongezi za pekee ziende kwa wataalamu wetu wa Sheria kutoka Afisi ya Baraza la Wawakilishi kwa jitihada zao kubwa walizozionyesha katika kuwapatia wajumbe wa Kamati hii maarifa kuhusu

mswada huu na kuwaelekeza mambo mbali mbali ambayo msingi wake ni kuufanya Mswada huu uwe bora zaidi.

**Mheshimiwa Spika;** Kamati ya Kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa ilikaa siku ya Tarehe 2 Disemba 2022 na kuupitia Mswada huu, kifungu kwa kifungu na kutoa mapendekezo mbalimbali kwa uweledi na umakini mkubwa kuhusiana na vifungu hivyo vilivyomo katika Mswada huu na hatimae kukubaliana na mapendekezo hayo. Hata hivyo, kamati inashauri wakati wa kuandaa miswada kama hii ya sheria mbalimbali kuwashirikisha watumiaji wa karibu wa sheria hizo ili kuwasilisha maoni yao wakati wa urekebishaji huo.

**Mheshimiwa Spika;** kabla ya kuendelea na mapendekezo ya Kamati yetu katika Mswada huu, naomba kuwatambua Wajumbe wanaounda Kamati hii kama ifuatavyo:

| | | |
|---|---|---|
| *1.* | Mhe. Machano Othman Said | Mwenyekiti |
| *2.* | Mhe. Mtumwa Peya Yussuf | Makamu Mwenyekiti |
| *3.* | Mhe. Salma Mussa Bilali | Mjumbe |
| *4.* | Mhe. Zaina Abdulla Salum | Mjumbe |
| *5.* | Mhe. Mohamed Mgaza Jecha | Mjumbe |
| *6.* | Mhe. Suleiman Makame Ali | Mjumbe |
| *7.* | Ndg. Ali Alawy Ali | Katibu, na |
| *8.* | Ndg. Mwanaisha Mohammed Kheir | Katibu |
| *9.* | Ndg. Amina Abeid Hemed | Mkalimani wa Lugha za Alama |

**Mheshimiwa Spika;** ikumbukwe kuwa, Mswada huu umejumuisha Sheria tano ambazo ni Marekebisho ya Sheria ya Fedha, namba 15 ya mwaka 1986 , Marekebisho ya Sheria ya Rufaa, namba 1 ya mwaka 2006, Marekebisho ya Sheria ya Mfuko wa Hifadhi ya Jamii, namba 2 ya Mwaka 2005, Marekebisho ya Sheria ya Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Maji na Nishati Zanzibar, namba 7 ya mwaka 2013 na Marekebisho ya Sheria ya Makampuni, namba 15 ya mwaka 2013. Ambazo kiujumla marekebisho katika vifungu vya Sheria hizi yamefanya ili kuondoa uzito wa utekelezaji unakumbana nazo.

**Mheshimiwa Spika;** naomba sasa uniruhusu nieleze baadhi tu ya marekebisho na mapendekezo ambayo Kamati yetu imeyafanya kutokana na Marekebisho yaliyofanywa katika Sheria hizi kuwa na ubora na kutumia utaalamu wa hali ya juu. Hivyo, Kamati yangu kazi yake imekuwa ndogo sana

katika kuupitia, kuujadili na kupendekeza kufanywa marekebisho ya kisarufi na misamiati iliyotumika pamoja ndani ya Mswada huu.

**Mheshimiwa Spika;** pia, naomba kuwatanabahisha Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza lako tukufu ya kwamba, hotuba hii inatoa ufafanuzi wa baadhi tu ya vifungu ambavyo vimependekezwa na kufanyiwa marekebisho na Kamati, hivyo maelezo zaidi ya mapendekezo hayo yamo katika muhtasari wa marekebisho yetu ambayo Waheshimiwa Wajumbe tayari mmeshapatiwa.

**Mheshimiwa Spika;** katika *sehemu ya pili* ya Mswada huu inayohusu Marekebisho ya Sheria ya Fidia kwa Wafanyakazi, Namba 15 ya 1986, Sheria hii imekuja kuhamisha fidia kwa baadhi ya mafungu ya wafanyakazi walioajiriwa katika sekta za umma au binafsi na ambao ni wanachama wa ZSSF na kuzipeleka fidia zao katika Sheria ya mfuko wa Hifadhi ya Jamii nam. 2 ya 2005. Kufuatia marekebisho hayo Kamati inashauri kifungu cha *4 (2)* cha Sheria hii, kurekebishwa kwa kuongeza maneno *"Jamuhuri ya"* baina ya neno "Serikali"na "ya" pamoja na kuingiza maneno "wa Tanzania" baina ya maneno *"Muungano"* na *"zilizopo"* ili kuonesha usahihi wa Serikali gani ya Muungano iliyotajwa katika kifungu hiki.

**Mheshimiwa Spika;** aidha, katika kifungu kidogo cha 4(3) kamati inashauri kufutwa kwa aya (a, b) ambacho kinaelezea fao la kuumia kazini pamoja na fidia inayotokana na kifo kilichotokana na utekelezaji wa kazi zao kwa kuwa maelezo ya mafao na fidia hizo zitaonekana moja kwa moja kwenye kanuni zitazotungwa na Mfuko wa Hifadhi ya Jamii Zanzibar.

**Mheshimiwa Spika;** katika *sehemu ya Tatu* ya Mswada huu inayohusiana na marekebisho ya Sheria ya Rufaa za Kodi Zanzibar, Namba 1 ya 2006. Kamati inashauri kufanywa marekebisho katika kifungu cha 25, kifungu kidogo cha *7* katika aya ya *(c)*, kwa kuongeza neno *"masharti"* baina ya neno *"ya"* na *"kifungu"* kwa lengo la kuweka sawa mtiririko wa maneno.

**Mheshimiwa Spika;** Katika sehemu ya Tano ya mswada huu inayohusiana na marekebisho ya Sheria ya Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Maji na Nishati, nam. 7 ya 2013 ambayo imekwenda kufuta kifungu cha 33,34 na 35 vya Sheria mama vinavyotokana na kuvunjwa kwa Baraza la kuwakilisha watumiaji, ambalo lilikuwa likisikiliza malalamiko ya watumiaji wa huduma za maji pamoja na kuzifikisha changamoto zinazotokana na watumiaji hao katika ngazi za juu zinatolewa malalamiko hayo. Aidha, kwa sasa kazi hizi zinafanywa na mamlaka husika ZURA kufuatia kuundwa kwa kitengo cha huduma kwa Wateja ambacho ndicho kinachopokea malalamiko mbalimbali yanayosiana na kazi walizokuwa wakifanya baraza hilo, kamati inashauri kukiimarisha kitengo hicho kwa kuweka huduma za moja kwa moja ili kuepusha usumbufu unaoweza kujitokeza kwa wananchi.

**Mheshimiwa Spika;** Sehemu ya Sita ya Marekebisho ya Sheria ya Makampuni Nam.15 ya 2013 ambayo inakwenda kufuta kifungu cha 238 (3) kwa sababu ya kurahisisha utekelezaji wa kisheria. Aidha, marekebisho haya ambayo yatakwenda kuruhusu sasa Kampuni ambazo zinasajiliwa Tanzania Bara hazitohitaji kufanyiwa usajili mwengine kwa upande wa Zanzibar na badala yake sasa Kampuni hizo zitaendelea na utaratibu mwengine uliowekwa.

**Mheshimiwa Spika;** Kamati yetu imeridhia marekebisho haya na kuliomba Baraza hili tukufu kuyazingatia mapendekezo ya Marekebisho yote ambayo kwa lengo la kuziboresha Sheria hizi pamoja na kuzipa nguvu ili ziweze kwenda sambamba na masharti ya kimataifa katika utekelezaji wake.

**Mheshimiwa Spika;** kwa kumalizia tunaiomba Serikali kuyazingatia na kuyafanyia kazi yale yote yaliyopendekezwa na Kamati na wadau kutoka taasisi mbalimbali ambazo kwa namna moja au nyengine wamesaidia kutoa maoni ambayo yatapelekea Sheria hizi kuwa na ubora zaidi katika utekelezaji wake. Kufanya hivyo ni kuisaidia Serikali na taasisi husika kuepuka udhaifu na migogoro isiyo ya lazima hali inayoweza kupelekea kutotekelezeka kwa Sheria hizo na kusababisha madhara kwa jamii na nchi yetu kwa ujumla.

**Mheshimiwa Spika;** baada ya kuelezea haya machache nawaomba Wajumbe wa Baraza lako tukufu, wenye hekma na busara waweze kutumia uweledi wao kuuchangia na kuurekebisha Mswada huu ulio mbele yetu kwa kutoa mawazo yatakayosaidia kiutendaji ili kuufanya uwe bora zaidi na hatimaye kuupitisha kwa kupata ufanisi.

**Mheshimiwa Spika; Nomba kuwasilisha**.

……………………………………………

***(Machano Othman Said)***
**Mwenyekiti**
**Kamati ya Kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa,**
**Baraza la Wawakilishi,**
**Zanzibar**